# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI - SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Machi 2025 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022**



## SALAM KUTOKA KWA MKURUGENZI



***Bw.Jimson Mhagama-Mkurugenzi Mtendaji-Same***

## *Tuendelee kuchukua Tahadhari dhidi ya Homa ya Mpox*



***Picha ikimuonesha mgonjwa wa Mpox***

***Nichukue nafasi hii kuwakumbusha wananchi wa Wilaya ya Same kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Mpox ambao***

*uliripotiwa kuingia nchini tangu mapema mwezi Machi 2025.*

*Ugonjwa wa Mpox huambukizwa kwa kugusa majimaji yoyote yanayotoka kwa mgonjwa hivyo inashauriwa kuepuka kukumbatiana, kushikana mikono na hata kusafisha nguo zilizotumiwa na mgonjwa wa Mpox.*

*Ugonjwa huu chanzo chake kilitokana na maambukizi kutoka kwa wanyama na kuingia kwa binadamu .*

*Machi 9, 2025 Waziri wa Afya Jenister Mhagama alitangaza kupatikana kwa wagonjwa wawili wa ugonjwa wa Mpox hapa nchini baada ya kukamilisha uchunguzi wa kimaabara.*

***Dalili za ugonjwa huu ni pamoja na homa, maumivu ya kichwa, upele, maumivu ya mgongo na misuli kuuma ,ugonjwa huu huambatana zaidi na upele ambao mara nyingi huanza kwenye uso kisha kuenea kwenye sehemu nyingine za mwili,ikiwemo viganja vya mikono na nyayo za miguu.***

*Katika kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Same wanajilinda dhidi ya ugonjwa huu tayari Idara ya Afya imeshatoa elimu kwenye mikusanyiko na makundi mbalimbali ikiwemo kwenye shule za Msingi na Sekondari, na elimu hii ni endelevu hadi maambukizi yatakapokoma hapa nchini.*

*Wilaya inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wananchi,tunahakikisha kila kwenye mkusanyiko wa watu tunatoa elimu kwani ni kupitia elimu tu ndipo tutaweza kuwaokoa wananchi dhidi ya maambukizi ya Mpox.*

*Nashauri iwapo mwananchi yoyote atapata dalili hizo awahi kituo cha afya kilicho karibu nae ili aweze kupatiwa matibabu.*

## RAIS DK.SAMIA SULUH U HASSAN AZINDUA MRADI WA MAJI SMK-AAGIZA WANANCHI WASAMBAZIWE MAJI KWA HARAKA.




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan akizindua Mradi Mkubwa wa Maji wa Same –Mwanga-Korogwe, kulia kwake ni Waziri wa Maji Mhe.Jumaa Aweso na aliye kwenye kiti-mwendo ni Waziri Mkuu Msataafu Ndg.Cleopa David Msuya.***

Machi 09,2025 ilikuwa ni siku muhimu na ya kihistoria kwa wakazi wa Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe pale Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alipozindua Mradi mkubwa wa Maji wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe uliogharimu shilingi bilioni 406 ambao unakwenda kumaliza tatizo la maji safi kwa wananchi wa Wilaya hizo ambao wamekabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu.

Mradi huu wa maji unatarajia kunufaisha jumla ya vijiji 38 vya wilaya za Same, Mwanga na Korogwe kwa kuwahakikishia huduma ya uhakika ya majisafi na salama.

Akizindua Mradi huo Dkt. Samia lisisitiza dhamira ya Serikali ya kuboresha huduma za kijamii hususan huduma ya majisafi, na kuongeza kuwa kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya mradi huo kumeongeza upatikanaji wa maji kutoka lita milioni 3.7

kwa siku hadi lita milioni 51.6 kwa siku, hatua inayotoa ahueni kubwa kwa wakazi wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe.

Alisema Mradi huo ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Same na Mwanga ambao tayari wameshaanza kunufaika na Mradi huo walioungojea kwa muda mrefu.

Mradi wa maji Same –Mwanga-Korogwe uliwekwa jiwe la msingi tarehe tarehe 12 Novemba, 2018 na Rais Samia akiwa Makamu wa Rais lakini baadaye utekelezaji wake ulisimama hadi pale Serikali ya Awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia ilipoamua kuufufua hadi sasa umeweza kuwanufaisha wananchi.

Rais Dkt. Samia ameagiza ulinzi na utunzaji wa miundombinu ya maji pamoja na vyanzo vya maji, ili huduma ya maji iwe toshelevu na endelevu.

Aidha Rais Dkt. Samia ameagiza Mamlaka ya Maji ya Same-Mwanga kuhakikisha inasambaza maji haraka majumbani,kwenye taasisi ambapo pia aliwataka wananchi kulipia Ankara za maji kwa wakati ili Mamlaka iweze kujiendesha na kutoa huduma ya uhakika ya maji.

Amewashukuru washirika wa maendeleo wakiwemo Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo wa OPEC (OFID), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait, na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (SFD) kwa kufanikisha utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe.

Kwa upande wake Waziri wa Maji Mhe.Jumaa Aweso (Mb) amesema Wizara ya Maji na watumishi wote wamejipanga kuhakikisha wanatimiza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, CCM (2020-2025), ambapo amesema mpaka sasa huduma ya maji vijijini imefika asilimia 83 kati ya 85 na mijini 91 kati ya 95 kama ilani hiyo inavyoelekeza kufikia Disemba, 2025.

Pia, Mhe. Jumaa Aweso amepiga marufuku huduma ya maji kukatwa siku za sikukuu na mwisho wa juma ili wananchi wafurahie huduma ya majisafi na salama ambayo wameisubiri kwa muda mrefu.

# MADIWANI SAME WAOMBA KUIDHINISHIWA BAJETI YA BIL.63.4



***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama akizungumza kwenye kikao cha Bajeti, kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Yusto Mapandde na Kulia kwake ni Afisa Serikali za Mitaa Mkoa wa Kilimanjaro Bw.Gasper Ijiko.***

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Same, limeomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 63.42 kwa mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo ndani ya wilaya hiyo.

Bajeti hiyo, ilijadiliwa katika Kikao Maalum cha Bajeti cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Januari 31,2025 kwa ajili ya kujadili na kupitisha mpango wa matumizi ya fedha kwa mwaka ujao wa fedha.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mheshimiwa Yusto Mpande amesema bajeti hiyo imelenga kuboresha na kuimarisha sekta mbalimbali za Maendeleo ndani ya wilaya ya Same ili kuimarisha ustawi wa wananchi wa Same.

Aliwataka madiwani, watendaji pamoja na viongozi wengine Wilayani Same kuhakikisha kuwa mapato yanapatikana ili Halmashauri iweze kutekeleza miradi iliyopitishwa katika bajeti hiyo.

Alisema kipaumbele kwenye Bajeti hiyo ni umaliziaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoishia kwenye maboma ikiwemo ya majengo ya shule, majengo ya miradi ya afya pamoja na mengineyo ili walengwa waweze kunufaika nayo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Same Bi. Upendo Wella amepongeza namna bajeti hiyo ilivyowasilishwa na kuwaomba madiwani pamoja na watendaji kuongeza nguvu katika ukusanyaji wa mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato kutokana na uwepo wa mahitaji mengi zaidi katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Diwani wa Kata ya Makanya, Damari Kingalu amesema kuwa bajeti hiyo imelenga zaidi kwenye miradi inayoigusa jamii moja kwa moja ikiwemo elimu, afya na usafirishaji huku akiwasisitiza wananchi kushiriki katika shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## KAMPENI YA MSAADA WA KISHERIA YA MAMA SAMIA IMEWAFIKIA WANANCHI ZAIDI YA 2000 WILAYANI SAME.



***Afisa Ardhi Mteule Wilaya ya Same Bi.Sampa Angelina akitoa elimu ya usawa katika umiliki wa ardhi kwa Wananchi wa Kijiji cha Kadando Kata ya Maore wakati Timu ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ilipofika kijijini hapo.***

Kampeni ya Mama Samia Legal Aid imetoa elimu kwenye Kata kumi za Wilaya ya Same ambapo pia ilisikiliza wananchi na kutatua migogoro mbalimbali ya wananchi na migogoro mingine imefikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya mama Samia imelenga kutoa elimu ya masuala mbalimbali ya sheria na kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi ambapo kesi zilizofikishwa Mahakamani wananchi wamepewa wanasheria wa kuwasimamia Mahakamani.

Akizungumza wakati alipofika kuaga Ofisini kwa Mkuu wa Wilaya Mratibu wa Kampeni hiyo Wilaya ya Same Bi.Happiness Rhobi alisema Kampeni hiyo imetimiza lengo la Mama Samia la kutoa Elimu ya Sheria na Msaada wa kisheria bure kwa wananchi wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni aliipongeza timu hiyo kwa kufanya kazi WIlayani Same akisema kuwa kuna changamoto nyingi za kisheria kwenye maeneo ya Vijiji lakini wananchi hawajui watapata wapi msaada.

Alisema Mama Samia Legal Aid imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi hasa wananchi wa Vijijini kwa

Kaulimbiu ya Kampeni hii inasema "Msaada wa kisheria kwa Haki,Usawa,Amani na Maendeleo"

Mama Samia Legal Aid inaratibiwa na kusimamia na Wizara ya Katiba na Sheria na kwenye Wilaya ya Same ilifikia Kata za Vumari,Maore,Ruvu,Mwembe,Mabilioni,Makanya,Hedaru,Makanya,Ndungu na Myamba.

## DC KASILDA AWAKUMBUSHA MAAFISA UTUMISHI KUSIMAMIA VEMA STAHILI ZA WATUMISHI

Mkuu wa Wilaya ya Same, Mheshimiwa Kasilda Mgeni, amewataka Maafisa Utumishi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa Watumishi wanapata stahili zao za kiutumishi kwa wakati ili kupunguza malalamiko yanayotokana na Watumishi wakiwemo walimu kucheleweshewa stahili zao.

Akizungumza katika kliniki ya kutatua changamoto za walimu (Samia Teacher's Mobile Clinic) iliyowakutanisha walimu kutoka Wilaya za Mwanga na Same, Mhe. Kasilda ameeleza kuwa changamoto nyingi wanazokutana nazo walimu zinaathiri utendaji wao wa kazi, hivyo kupunguza ubunifu na ufanisi.

"Walimu wanapokumbwa na changamoto katika upatikanaji wa stahili zao na utendaji wao lazima ushuke hakutakuwa na ubunifu, na hali hii inaathiri ubora wa elimu"amesema.

Baadhi ya changamoto ambazo walimu waliwasilisha ni pamoja na kucheleweshwa kupandishwa madaraja, kubadilishiwa miundo baada ya kujiendeleza, malimbikizo ya mishahara, madai ya muda mrefu ya stahiki za uhamisho pamoja na madai ya kustaafu.

Timu inayojumuisha wataalam kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa (TAMISEMI) wakishirikiana na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) imefika Wilayani Same na kusikiliza kero mbalimbali za walimu na kuzipatia ufumbuzi.

Kwa upande wake makamu wa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Suleiman Ikomba ameishukuru Serikali kwa kuwa sikivu na kuunda klinik hiyo ambayo utasaidia kutatua changamoto za w

## MIL.402.7 ZA SWASH ZABORESHA MIUNDOMBINU YA AFYA




***Moja ya Vyoo vilivyojengwa chini ya Mradi wa SWASH***

Wilaya ya Same imepokea Shilingi Milioni 402.7 kutoka Miradi wa SWASH kwaajili ya Utekelezaji wa Miradi ya huduma za maji na Usafi wa Mazingira Vijijini-SRWSSP ambapo fedha hizo zimenufaisha jumla ya Zahanati 10 Wilayani humo.

Akizungumzia Miradi hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Be.Jimson Mhagama amesema fedha hizo zimepokelewa kwa awamu tatu mfululizo.

Amesema awamu ya kwanza Wilaya ilipokea Shilingi Mil.160.7 ambazo zilinufaisha Zahanati nne na awamu ya pili zilipokelewa Shilingi Mil.200 ambazo zilinufaisha Zahanati tano."Awamu ya tatu tumepokea milioni 42 ambazo zimeelekezwa kujenga

miundombinu ya maji na Usafi wa Mazingira kwenye Zahanati ya Mbakweni"alisema Bw.Mhagama.

Akitoa mchanganuo kuhusu matumizi ya fedha hizo Afisa Afya na Usafi wa Mazingira wa Wilaya ya Same Bi.Yuster Malisa alisema fedha zilizotolewa awamu ya kwanza zilitumika kwenye Zahanati nne ambapo kila Zahanati ilijengewa vyoo,mnara wa kuweka tenki la maji,kichomea taka (incenereta) ,vinawia mikono na shimo la majivu na kutupa kondo la nyuma la mama.

"Awamu hii ilinufaisha Zahanati za Masandare,Makanya Kitivo,Kitivo na Ruvu Kombo"alifafanua Bi.Malisa na kuongeza kuwa Zahanati zilizonufaika awamu ya pili kuwa ni Kadando, Kihurio, Kasapo, Suji Malindi na Saweni.

Amesema kuwa katika awamu ya tatu ambapo Wilaya imepokea Mil.42 zilielekezwa Zahanati ya Mbakweni ambapo imetumika kujenga vyoo, kichomea taka, mnara wa tenki la maji,shimo la kutupa majivu na la kutupa kondo la nyuma.

## BODI MPYA YA AFYA YATAKIWA KUWA CHACHU YA KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA



***Wajumbe wa Bodi mpya ya Afya Wilaya ya Same wakiwa kwenye picha ya pamoja na Katibu Tawala WIlaya ya Same Bi.Upendo Wella (Mwenye miwani) . Walioketi kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Bodi Mchungaji Muberwa Buchwechwe, Mganga Mkuu wa WIlaya Dkt.Alex Alexander na Kaimu Mkurugenzi Dkt.Cainan Kiswaga.***

Wilaya ya Same imezindua Bodi Mpya ya Afya ya Wilaya hiyo ambayo itatumika kwa miaka mitatu kusimamia huduma za Afya Wilayani Same.

Akizindua Bodi hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya,Katibu Tawala wa Wilaya ya Same Bi.Upendo Wella aliitaka Bodi hiyo iwe chachu ya kuboresha huduma za afya.

"Tunaitegemea sana Bodi hii katika kuleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya afya,mjitahidi pia kutoa motisha kwa Watumishi wanaofanya vizuri"alisema Bi.Upendo.

Bodi hiyo iliyozinduliwa Februari 10,2025 inaongozwa na Mwenyekiti Mchungaji Muberwa Buchwechwe ambaye pia ni Msimamizi Mkuu wa Huduma za Afya wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Pare.

Mchungaji Buchwechwe ameshukuru kwa kuaminiwa kuitumikia nafasi hiyo na kuahidi kufanya kazi kwa weledi

Akitoa taarifa fupi ya huduma za AFya WIlayani humo kwa mwaka uliopita, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same Dkt.Alex Alexander amesema kwa mwaka 2024 Idara ya Afya Wilayani humo ilifanikiwa kutoa huduma ya usafirishaji wa dharura kwa kinamama wajawazito 326 na watoto 62 na kuwawezesha kufikia huduma za afya.

"Idara pia ilifanikiwa kufikia asilimia 100 ya ukusanyaji mapato lindwa ambapo Kwa upande wa Utekelezaji wa Mkataba wa Afya za lishe Wilaya imefanikiwa Kwa asilimia 97" amesema Dkt.Alex.

Kwa upande wa upimaji virusi vya UKIMWI na ushauri nasaha Wilaya ya Same Kwa mwaka 2024 ilipima watu 38,164 ambapo kati yao 532 waligundulika kuwa na maambukizi na wameanzishiwa dawa za kufubaza virusi ARV.

Dkt.Alex alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Kwa kunipatia Wilaya ya Same magari manne ya wagonjwa (Ambulance )ambazo zinatumika hospitali ya Wilaya,hospitali ya Mji na kwenye vituo vya Afya.

## WILAYA YA SAME KUAZISHA RADIO"*Same fm'*

Halmashauri ya Wilaya ya Same ipo katika hatua za mwisho za uanzishwaji wa Radio ya Jamii itakayojulikana kama ***Same Fm,*** uanzishwaji wa Radio hii unafadhiliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambapo kwa sasa tayari UCSAF wameshajenga mnara wa kupokea na kusambaza matangazo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama amesema ufadhili wa UCSAF unajumuisha ujenzi wa Mnara wa Matangazo pamoja na kujenga Studio za Kisasa.

Amesema tayari Halmashauri imeshapitia na kuridhia Hati ya Makubaliano (MoU) wa Uendeshaji na Usimamizi wa Mnara wa kupokea na kurushia matangazo uliojengwa na UCSAF Wilayani hapa,

Wilaya ya Same inatoa shukrani za dhati kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) kwa kuridhia kufadhili ujenzi wa Mnara na studio za kisasa Wilayani hapa ambazo zitafanikisha uanzishwaji wa Radio ***Same fm.***

Uanzishwaji wa Radio hii utasaidia katika kuhakikisha kuwa wananchi wa maeneo yote ya Wilaya ya Same na maeneo ya jirani wanafikiwa na taarifa mbalimbali za maendeleo kwani kwa sasa matangazo ya Radio hayafiki kwenye maeneo mengi ya Wilaya ya Same.

## WILAYA YA SAME YAOMBA WIZARA YA KILIMO KUSAIDIA UPATIKANAJI WA MICHE YA PARACHICHI



Kufuatia mahitaji makubwa ya miche ya zao la Parachichi Halmashauri ya Wilaya ya Same imeandika maombi Wizara ya Kilimo kuomba kusaidiwa miche 56,289 ya Parachichi zinazokomaa muda mfupi ili kuweza kuisambaza kwa wananchi.

Tangu mwaka 2022 Wilaya ya Same imeliweka zao la Parachichi kmiongoni mwa mazao ya kimkakati ya kuinua uchumi wa Wananchi wa ukanda wa milimani kwenye Wilaya ya Same.

Baada ya zao hilo kutangazwa kama zao la kimmkakakti lenye lengo la kuinua uchumi wa Wakulima tayari jumla ya miche 5,822 imeshaoteshwa kenye maeneo mbalimbali ambapo miche hiyo ilitolewa na wafadhili mbalimbali wakiwemo Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) pamoja na Shirika la Forest Focus.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya WIlaya ya Same Bw.Jimson Mhagama amesema mwamko wa wananchi kuotesha Parachichi zinazokomaa muda mfupi ni mkubwa sana ndio maana tumeamua kuomba Msaada wa Wizara ili kupata miche zaidi.

“Tuna Kata zaidi ya 12 za ukanda wa milimani ambao una baridi ambapo utafiti umeonyesha kwamba hizi Parachichi zinaweza kustawi na tayari wananchi tumewahamasisha kupanda parachichi hizi na mwamko umekuwa mkubwa” alisema Mhagama.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mheshimiwa Yusto Mapande ameahidi kufuatilia maombi hayo ya Miche Wizara ya Kilimo ili wananchi waweze kupatiwa.

Afisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Wilaya ya Same, Dkt.Cainan Kiswaga alisema miche ya Parachichi inayokomaa mapema ni chachu ya kuinua wananchi kiuchumi kwani mti mmoja wenye miaka mine unaweza kuzaa matunda 400 kwa mwaka na uzalishaji huongezeka kwa kadri umri wake unavyoongezeka ambapo mti wa miaka saba huzaa matunda hadi 800 kwa mwaka wakati miti ya asili ina uwezo wa kuzaa matunda 150 tu kwa mwaka.

Alizitaja Kata ambazo zao la Parachichi linastawi kuwa ni pamoja na Mshewa,Mhezi,Msindo,Vuje,Mtii,Bombo,Bwambo,Mpinji,Chome,Vudee, Vunta, Suji na Myamba.

# UZALISHAJI WA MKONGE SAME KUFIKIA TANI 2,500



*Moja ya shamba la Mkonge uliostawi*

Wilaya ya Same imejipanga kuongeza uzalishaji wa zao la Mkonge kutoka Tani 1,351 za sasa hadi kufiki tani 2,500 mwaka 2030 ili kupanua wigo wa upatikanaji wa mazao ya Viwanda na kuinua wananchi kiuchumi.

Zao la Mkonge ni zao la kimkakati kwenye Wilaya ya Same ambapo tayari Wilaya imetenga Ekari 4,000 kwenye Kata ya Makanya lenye vitalu 162 ambapo tayari vitalu 158 vimeshakodishwa kwa wawekezaji wa ndani ili kuongeza mapato ya Halmashauri.

Afisa Kilimo, Uvuvi na Mifugo wa Wilaya ya Same Dkt. Cainan Kiswaga amesema vitalu hivyo vimekondihwa kwa wadau 121 wa zao la Mkonge na vitalu vine vimetengwa kwaajili ya uzalishaji wa miche ya Mkonge ili kurahisisha upatikanaji wa miche.

Uanzishwaji wa zao la Mkonge kama zao la kimkakati unatokana na agizo la Waziri Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa ambapo alielekeza kila Wilaya hapa nchini kuwa na mazao ya kimkakati ili kukwamua wananchi kiuchumi.

“Tunaishukuru sana Bodi ya Mkonge hapa nchini kwa kutupatia miche 135,000 ya Mkonge ambayo imeweza kufikia wakulima 25 wa Mkonge kutoka Kata za Makanya,Saweni na Hedaru” alisema Dkt. Kiswaga.

Amesema kuwa katika kurahisisha uendeshaji na usimamizi wa uzalishaji wa zao la Mkonge Halmashauri imesimamia uanzishwaji wa ushirika wa Wakulima wa mkonge unaojulikana kama SAME SISAL AMCOS.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



***Mkuu wa Wilaya ya Same mheshimiwa Kasilda Mgeni (kulia) akifanya ziara ya kikazi kwenye bwawa la nyumba ya Mungu ambalo ni Chanzo kikuu cha Mradi wa Maji Same- Mwanga- Korogwe.***



***Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande akiendesha moja ya vikao vya Madiwani ambapo pamoja na mambo mengine amewasisitizia watumishi na Madiwani kupima Homa ya Ini (Hepatitis B) ili waweze kupatiwa chanjo ya kinga dhidi ya ugonjwa huo.***



***Pochi ya Mama Samia ilipofunguka na kuondoa kero ya makazi ya walimu.***

***Hili ni jengo jipya la Nyumba ya Walimu (2 in 1) lililojengwa kwenye shule ya Sekondari Angallah Kairuki kwa fedha shilingi Milioni 98.Nyumba kama hizi zimejengwa pia kwenye Shule za Sekondari Mighareni,Misufini-Goma,Malindi,Kalemawe na Kihurio Shule ya Amali.***




***Mwalimu wa Shule ya Msingi Mng'ende(kushoto) akipokea cheti cha pongezi kutika kwa Mkuu wa Wilaya Mhe.Kasilda Mgeni baada ya shule hiyo kufanya vizuri kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka 2024.Cheti hicho kilitolewa wakati wa kikao cha Tathmini ya Elimu Wilayani humo.***



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138,SAME**

**Mhariri Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Machi 2025 www.samedc.go.tz  email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***